Msiape kwa masanamu, wala kwa baba zenu

Imepokelewa kutoka kwa Abdillahi bin Omari- radhi za Allah ziwe juu yake- Amesema: Amesema: Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Msiape kwa masanamu, wala kwa baba zenu"

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Mtume rehema na amani ziwe juu yake amekataza kuapa kwa mashetani, yaani wingi wa shetani, nayo ni masanamu waliyokuwa wakiyaabudu washirikina badala ya Mwenyezi Mungu, na ndiyo yalikuwa sababu ya ujeuri wao na ukafiri wao. Anakataza rehema na amani ziwe juu yake kuapa kwa baba za mtu; Ilikuwa ni desturi ya Waarabu katika zama za kabla ya Uislamu kuapa kwa baba zao kwa kujifaharisha na kwa kuwatukuza.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/8959